

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA
MAKUNDI MAALUM

Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346

Nukushi: +255 (026) 2963348

Barua Pepe: ps@jamii.go.tz

Tovuti: www.jamii.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P 573,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

YAH; SHUKRANI KWA MHE. RAIS KUKUBALI KUTUMIA MAJENGU YA *WORLD VISION*
KUWA CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII

03 Agosti, 2024

Ndugu Wananchi, Wizara inayo furaha kupokea maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwamba, majengo yaliyokuwa ya Shirika linaloshugulika na kupunguza umasikini kwenye familia na jamii *World Vision* katika Wilaya ya Gairo, sasa yatumike kutoa huduma za Chuo cha Maendeleo ya Jamii.

Maelekezo hayo yametolewa na Mhe. Rais tarehe 2 Agosti, 2024 akiwa katika ziara ya kikazi wilaya ya Gairo, katika mkoa wa Morogoro.

Ndugu Wananchi, Wizara imeanza kufanya kazi maelekezo haya kwa kuratibu wadau wote stahiki kwenye utekelezaji huu ili majengo haya yakabidhiwe na mipango ya kuwezesha Chuo hicho kuanza kazi ianze.

Baadhi ya Wadau washirika kwa uchache ni pamoja na Wizara za Kisekta, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Gairo na Wawakilishi wa Wananchi Gairo.

Wizara inatoa Shukrani za Dhati kwa Mhe Rais kwa kuendelea kujenga imara Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwani ndiyo injini ya maendeleo kutohakana na kwamba, inahusika kwenye kuchochaea Ari na mabadiliko chanya ya fikra za jamii ili kujiletea maendeleo na ustawi endelevu.

Gwajima

Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM.